

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
ADVANCED CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION
EXAMINATION

121/1

KISWAHILI 1

(Kwa Watahiniwa Walioko Shulenii na Wasiokuwa Shulenii)

Muda: Saa 3

Jumatatu, 11 Februari 2013 asubuhi

Maelekezo

1. Karatasi hii ina maswali **kumi (10)** katika sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali **saba (7)** kwa kuzingatia maelekezo kutoka katika kila sehemu.
3. Kila sehemu ina alama **ishirini (20)**.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Vikokotozi **haviruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
6. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu cha kujibia.



Ukurasa wa 1 kati ya kurasa 4

SEHEMU A (alama 20)

UFAHAMU

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

1. Soma shairi lifuatalo kwa makini kisha jibu maswali yanayofuata:

Mimi naitwa muhogo, nani asiyenijua?
Pato hata liwe dogo, ubora nashikilia,
Sijui tega mtego, ni mshindi asilia,
Muhogo ndiye rafiki, nikufaaye kwa dhiki.

Watu walionifuja, kwa nia na pambazuko.
Wakati ulipokuja, walipata hangaiko,
Kwa njaa walinitaja, wakihofu **pukutiko**,
Muhogo ndiye rafiki, nikufaaye kwa dhiki.

Palipo kame naota, mimi siyo mbamia,
Na sitofanya matata, ukininyima mbolea,
Baridi inayotata, kwangu mbali yapitia,
Muhogo ndiye rafiki, nikufaaye kwa dhiki.

Hebu tafuna muhogo, maji **ukigugumia**,
Au uchome muhogo, kwa chai ukatumia,
Lau chemsha muhogo, safarini kujilia,
Muhogo ndiye rafiki, nikufaaye kwa dhiki.

Ifikapo Ramadhani, mwezi tunaotubia,
Zaidi chakula gani, **kaumu** wategemea,
Nimo ndani futarini, wengi wanifuturia,
Muhogo ndiye rafiki, nikufaaye kwa dhiki.

Nikija kwenye ugali, nani asofurahia?
Ni laini kwa asili, kisu hutaulizia,
Wanga wangu kwenye mwili, nguvu utakupatia,
Muhogo ndiye rafiki, nikufaaye kwa dhiki.

Chukua unga ukande, ongeza sukari haba,
Kata biskuti pande, uvioke kwa vibaba,
Ni biskuti vipande, utazila kwa mahaba,
Muhogo ndiye rafiki, nikufaaye kwa dhiki.

Ninayo mboga makini, kisamvu nakutajia,
Kina nyangi vitamini, za muhimu kwa afya,
Chakula utathamini, kisamvu ukitumia,
Muhogo ndiye rafiki, nikufaaye kwa dhiki.

Shina langu ni **shani**, kuni utajipatia,
Mapishi ya kila fani, vyunguni kujiivia,
Utakuwa gharamani, mafuta ukizoea,
Muhogo ndiye rafiki, nikufaaye kwa dhiki.

Nimefikia **hatima**, mbele sitaendelea,
Kutenda siyo kusema, ubingwa nauwania,
Ibuka ulipozama, nikuone waelea,
Muhogo ndiye rafiki, nikufaaye kwa dhiki.

Maswali

- (a) Eleza mawazo makuu matatu yanayotokana na shairi hili.
 - (b) Eleza manufaa matano ya muhogo yaliyoelezwa katika shairi ulilosoma.
 - (c) Andika kichwa cha shairi hili kwa maneno matatu tu.
 - (d) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyatumbika katika shairi hili:
 - (i) Pukutiko
 - (ii) Ukgugumia
 - (iii) Kaumu
 - (iv) Shani
 - (v) Hatima
 - (e) “Atekaye maji mtoni, asimtukane mamba.” Unafikiri methali hii inawakilisha wazo la ubeti upi katika shairi hili? Fafanua jibu lako ukihusisha maana na matumizi ya methali hiyo.
2. Andika ufupisho wa shairi ulilosoma katika swali la kwanza (1) kwa aya moja tu yenye maneno yasiyozidi mia na hamsini (150) na yasiopungua mia moja (100).

SEHEMU B (alama 20)

MATUMIZI YA SARUFI NA UTUMIZI WA LUGHA

Jibu maswali **mawili** (2) kutoka sehemu hii.

3. Eleza maana tano za neno “Chungu,” na kwa kila maana tunga sentensi moja inayofafanua maana hiyo.
4. Kwa kutumia mifano, fafanua tofauti tano zilizopo kati ya lugha ya kuzungumza na lugha ya kuandika.
5. Kwa kutumia mifano, toa hoja mbili kuonesha ubora na hoja tatu kuonesha udhaifu wa kuainisha ngeli za nomino kwa kigezo cha kimofolojia.
6. (a) Elezea umuhimu wa aina tatu wa nomino za Kiswahili.
(b) Onesha miundo mitano ya kiima katika tungo na kwa kila muundo toa mfano dhahiri.

SEHEMU C (alama 20)

UTUNGAJI

Jibu swali la saba (7).

7. Jifanye wewe ni mionganini mwa wafanyakazi waliopunguzwa kazi katika kiwanda cha Chai kilichopo Mufindi. Kwa bahati nzuri Kampuni ya Usambazaji Sukari imetangaza nafasi ya ajira ya wakala wa usambazaji sukari. Andika wasifu binafsi utakaoutuma katika kampuni hiyo. Jina lako liwe Hamsini Uhuru.

SEHEMU D (alama 20)

MAENDELEO YA KISWAHILI

Jibu swali **moja** (1) kutoka schemu hii.

8. Kwa kila nchi, eleza njia nne zilizosaidia kuenea kwa Kiswahili katika nchi ya Rwanda na Burundi kabla na baada ya uhuru.
9. Taasisi mbalimbali ziliundwa baada ya uhuru ili kukikuza na kukieneza Kiswahili nchini Tanzania. Fafanua kazi nne za Taasisi ya Elimu Tanzania na nne za Chama cha Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

SEHEMU E (alama 20)

TAFSIRI

Jibu swali la **kumi** (10).

10. Kwa kutumia mifano, fafanua mambo sita yanayosababisha upungufu katika tafsiri.